SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU

TANGAZO LA SERIKALI NA. ..... TAREHE .....

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA NO. 29)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 na. 16

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU)
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, 2017

Jina, mipaka na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za Ada na Ushuru) 2017, zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali na zitatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

2. Katika sheria ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri na mtoa huduma kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.Malipo hayo yanahusisha pia ushuru wa mazao unaotozwa na Hallmashauri kwa kutumia Wakala au Halmashauri yenyewe.

"Afisa Muidhiniwa" Maana yake ni Afisa au mtumishi wa Halmashauri aliyeteuliwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

" Gulio" Ni sehemu au eneo lililotengwa na Halmashauri kama ilivyooneshwa katika jedwali la sheria ndogo hizi kwa shughuli za kuuza na kununua mazao ya kilimo na mifugo pamoja na bidhaa mbalimbali za mahitaji ya binadamu.

"Kibanda" maana yake ni jengo au chumba cha biashara ndani ya eneo la Halmashauri

"Kizimba" maana yake ni eneo lililopo ndani ya eneo la

soko linalotumiwa na wafanyabiashara kuuzia bidhaa mbalimbali lenye ukubwa mita nne za mraba.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia mifugo mbalimbali.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa pamoja na afisa yeyote wa Halmashauri atakayekuwa ana kaimu nafasi ya Mkurugenzi.

"Meza" maana yake ni meza zinazotumiwa na wafanya biashara kuuzia bidhaa katika jengo au eneo la Halmashauri.

"Soko" Maana yake ni eneo lolote lile lililoanzishwa na kuendeshwa na Halmashauri kama eneo la kuuzia na kununulia bidhaa au huduma kufuatana na taratibu zilizowekwa na Halmashauri.

"Wakala" maana yake ni mtu atakayeteuliwa na Halmashauri kwa lengo la kukusanya ada na ushuru na kutekeleza sheria ndogo hizi.

Utozaji wa Ada na Ushuru

3. Kutakuwa na ada na ushuru kwa huduma, biashara mbalimbali utakaotozwa na kukusanywa na Halmashuri/wakala kwa mtoa huduma au mfanyabiashara katika Halmashauri,

(a) Kwa ajili ya vibali, leseni, mazao, huduma na biashara mbalimbali zinazotolewa ndani ya Halmashauri. Kama zilivyooneshwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

(b) Isipokuwa kwa malipo ya ada zinazolipwa kwa muda maalum, ada na ushuru utakaotozwa katika sheria ndogo hizi, utalipwa kwa Halmashauri au wakala kabla au mapema mara baada ya huduma au biashara kuanza.

(c) Stakabadhi yenye nembo ya Halmashuri itatolewa na afisa mwidhiniwa/wakala kwa mtoa huduma/mfanyabiashara kulingana na kiasi cha fedha kilicholipwa.

(d) Itakuwa ni haki ya mtu yeyote atakayelipia ushuru na ada kudai risiti ya malipo halali kwa Halmashauri au wakala.

(e) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubadilisha viwango vya ada na ushuru, muda wowote kadri itakavyoona inafaa kufanya hivyo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na sheria.

(f) Tarehe ya mwisho ya kulipia ada na ushuru chini ya sheria ndogo hizi itakuwa tarehe 28 hadi 30 ya kila mwezi, isipokuwa kwa ada na ushuru zinazolipwa kwa mwaka tarehe ya mwisho itakuwa ni 30 Juni ya kila mwaka baada ya hapo Halmashauri itakuwa na haki ya kudai riba ya asilimia 1.5 ya ada na ushuru unaodaiwa vitakavyolipwa kwa pamoja na mdaiwa.

Viwango vya shuru na ada mbalimbali

5. Halmashauri itatoza ushuru na ada kwa viwango mbalimbali kama ilivyooneshwa katika safu A-H za jedwali katika sheria ndogo hizi.

Uteuzi wa Wakala

6. Halmashauri inaweza kukusanya ushuru na ada kwa kumteua

(a) Wakala atakayeteuliwa chini ya sheria ndogo hizi atakusanya ada na ushuru kwa wakati na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati uliokubalika kwenye mkataba.

(b) Wakala atatoa taarifa ya maandishi ya majina ya wtu waliolipa ushuru/ ada,kiasi kilichotolewa kwa wakati na majina ya watakoshindwa kulipa kwa wakati kwa Halmashauri kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kisheria watakaoshindwa kutekeleza wajibu wao.

(c) Malipo ya Wakala yatalipwa kwa makubaliano ya Mkataba kati ya Halmashauri na wakala kulingana na kazi/makusanyo aliyofanya wakala.

Makosa kwa wakala

7 Itakuwa ni kosa kwa wakala;

a) kushindwa/kutokuwasilisha kwa Halmashauri kiasi chochote cha pesa za ada na ushuru uliokusanywa .

b) Kumtoza mtu ada/ushuru kiasi kinachozidi au kinachopungua kile kilichowekwa kwa mjibu wa sheria ndogo hizi.

c) Kwa uzembe au kwa kufahamu kutoa taarifa za uongo kwa mdomo au kwa maandishi juu ya ushuru/ada alichokusanya au juu ya idadi ya majina ya walipa ushuru.

Ukusanyaji wa madeni

8. (a) Mtu yeyote atakayekwepa kulipa ada na ushuru atachukuliwa hatua za kisheria na wakala akishirikiana na Halmashauri au kama hakuna wakala basi Halmashauri yenyewe.

(b) Ikiwa mtu yeyote anayepaswa kulipa ada na ushuru atashindwa kutekeleza wajibu wake wa kulipa ada na ushuru unaostahili kulipa, Halmashauri inaweza kukusanya ada na ushuru huo kupitia/kwa kumtumia dalali wa mahakama ikiwa ni pamoja na kufunga biashara ya mdaiwa mpaka atakapokuwa amelipa deni.

(c) Bila kuathiri masharti ya kifungu (6) (a) (b),

Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada na ushuru kwa kukamata na kushikilia mali zinazohamishika zinazomilikiwa na mdaiwa zenye thamani sawa na ada na ushuru unaodaiwa.

(d) Endapo zitapita siku thelathini tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa bila mdaiwa kulipa deni, Halmashuari itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada.

9. Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokana na kukamatwa kwa mali za mwenye deni wakati wa kukusanya katika maeneo husika na kushikiliwa mali hizo na Halmashauri.

10. Afisa Mwidhiniwa au wakala atakuwa na mamlaka ya kuingia mali popote ambapo biashara inafanyika au panapotolewa huduma katika eneo la Halmashauri, wakati wowote na kufanya ufuatiliaji na ukaguzi kwa nia ya kukusanya ada na ushuru.

Makosa na Adhabu

11. Mtu yeyote ambaye:

a) Atapuuza au atashindwa/kuwasilisha/kulipa ada au ushuru unaopaswa kulipwa katika sheria ndogo hizi au

b) Atasababisha ada na ushuru unaopaswa kulipwa katika sheria ndogo hizi, kutolipwa na mtu anayepaswa kulipa kwa namna yeyote ile isiyo na sababu ya msingi au

c) Atashindwa kuwasilisha/kulipa ada au ushuru huo kwa wakati kwa mujibu wa sheria ndogo hizi au

d) Atashindwa kutunza kumbukumbu au taarifa zinazohusiana na ada na ushuru uliotozwa na kukusanywa au

e) Atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa ada na ushuru.

Atakuwa ametenda kosa katika sheria ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Tshs. elfu hamsini (50,000) kwa kila kosa au kifungo cha miezi sita jela au atapewa adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifisha kosa

12 Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufifisha kosa iwapo mkosaji atakiri kosa na atatozwa faini kwa mujibu wa sheria ndogo hizi, pamoja na kulipa deni la ada na ushuru unaodaiwa.

JEDWARI

SEHEMU A.

ADA YA KUWEKA VIBAO VYA MATANGAZO.

Ada ya fomu ya maombi ya kibali cha kuweka bango
la tangazo/matangazo ya biashara……10,000 kwa kila ombi.

a) Mabango yasiyong'aa……5,000 kwa mita moja ya mraba kwa mwaka.
b) Mabango yanayoang'aa……..8,000 kwa mita moja ya mraba kwa mwaka.
c) Matangazo yabiashara…….10,000 kwa siku siku 1-7
d) Matangazo mengineyo……..5,000 kwa bango kwa eneo.
e) Matangazo ya biashara kwa
kutumia vipaza sauti……25,000 kwa siku moja.

SEHEMU B.

ADA YA KUKODI UKUMBI NA MALI ZA HALMASHAURI.

a) Ukumbi wa Halmashauri…… 300,000 kwa siku moja.
b) Viti vya ukumbini……300 kwa kiti kwa siku.
c) Lori la Halmashauri…….200,000 kwa siku moja.
d) Mitambo ya Halmashauri Trekta,Rola,Boza)……250.000 kwa siku moja.
e) Greda la Halmashauri……..750,000 kwa siku

SEHEMU C

USHURU WA MAZAO YATOKANAYO NA SHUGHULI ZA UVUVI.

Ushuru wa mizigo ya samaki;

a) Samaki tenga la kg 100……5,000.
b) Samaki tenga la kg 50……..2,000.
c) Mabondo ya samaki kg 100……..2, 000.
d) Mabondo ya samaki kg 50…….. 1,000.
e) Lori lenye mzigo wa samaki/dagaa.....……10,000 kwa siku.

SEHEMU D

USHURU WA HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA HALMASHAURI

a) Huduma zinazotolewa na wazabuni , kandarasi , kampuni/tawi la kampuni na watu binafsi
……0.3% ya mapato ya huduma kwa mwaka
b) Huduma zitolewazo na mawakala;
    i) TBL……..2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja.
    ii) CRDB……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja.
    iii) NBC……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja
    iv) TPB……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja
    v) NMB……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja
    vi) TUNAKOPESHA LTD……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja
    vii) FAIDIKA……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja
    viii) Bima……2% ya gharama ya huduma kwa mwezi mmoja

SEHEMU E

A: ADA YA UPIMAJI VIWANJA NA UTAYARISHAJI HATIMILIKI ZA KIMILA.

a) Viwanja/shamba lisilozidi ekeri 10……50,000 kwa kiwanja/ shamba.
b) Viwanja/shamba linalozidi ekeri 10……250,000 kwa kila ekari kumi zinazoongezeka.

B: ADA YA KUUZA VIWANJA VYA HALMASHURI VILIVYOPIMWA

NA	**MATUMIZI YA KIWANJA**	**BEI KWA MITA MRABA**
1	Makazi	2,000,000
2	Makazi/Biashara	2,300,000
3	Biashara	2,500,00
4	Huduma za Jamii	2,000,00

SEHEMU F

USHURU WA MAZAO YA MISITU

a) Asali kwa lita moja ……6,000.
b) Nta kwa lita moja ……..4,000.
c) Kuni tani moja……..3,000
d) Kuni kwenye baiskeli/mkokoteni……1,500
e) Mbao……100 kwa ubao mmoja
f) Magogo……3000 kwa kila gogo
g) Nguzo ……3000 kwa nguzo moja
h) Mkaa……7200 kwa gunia

SEHEMU G

USHURU WA VIBANDA VYA BIASHARA

a) kuzunguka gulio/soko la Halmashauri……10,000 kwa mwezi.
b) Kuzunguka vituo vya mabasi……..10,000 kwa mwezi.
c) Pango la meza katika soko la halmashuri……5,000 kwa mwezi.
d) Ushuru wa kizimba……1000 kwa kila siku ya gulio.

SEHEMU H

ADA/USHURU UTALII KATIKA HIFADHI YA WANYAMA PORI KWA WATARII WA NDANI.

a) Gari linaloingia katika eneo la hifadhi……10,000 kila gari kwa siku 14 .
b) Makambi ya watalii ……5,000 kila mtalii kw siku moja.

SEHEMU I

USHURU WA MAWE NA MCHANGA NA TOFARI

a) Lori la mawe /kokoto ……..5,000 kwa trip
b) Lori la mchanga……... ……...5,000 kwa trip
c) Lori la tofari……5,000 kwa trip

SEHEMU J

USHURU WA MAZAO YA KILIMO NA MATUNDA

a) Mpunga…… 2000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
b) Mahindi/Mtama…… 1000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
c) Alizeti…….1500 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
d) Maharage……4000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
e) Ufuta……4000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
f) Nyanya/tango/embe/papai/pilipili hoho /nyanya chungu…….500 kwa tenga
g) Mahindi mabichi …..35,000 kwa Canter na 50,000 kwa Fuso
h) Karanga zilizobanguliwa…….. 3000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
i) Karanga zisizobanguliwa…….1500 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
j) Njegere mbichi/Kunde……..1000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
k) Viazi vitamu/Mviringo…….1000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi
l) Vitunguu……2000 kwa gunia au asilimia isiyozidi 5 ya bei ya manunuzi

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umebandikwa katika sheria ndogo hizi kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika tarehe…….mwezi……201.. mbele ya ;

……
ROBERT MASUNYA
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAY A YA IRINGA.

…….
STEPHEN MHAPA
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

NAKUBALI

……
MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE (MB)
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

DODOMA,

TAREHE……..MWEZI……2017.

HALMASHAURIYA WILAYA YA IRINGA

Mheshimiwa mwenyekiti ,
Kamati ya fedha utawala na mipango.

Halmashauri kupitia kitengo cha sheria imeandaa rasimu ya sheria ndogo ya ada na ushuru kwa huduma na biashara mbalimbali zinazotolewa na wazabuni,wakandarasi,mawakala na wafanya biashara mbaalimbali ndani ya Halmashauri.
Rasimu inaonesha ushuru na ada katika; kuweka vibao vya matangazo ndani ya Halmashuri,kukodi mali za Halmashauri, ushuru wa mazao ya samaki, ada kwa mawakala wa bima, mabenki na taasisi za fedha zinazotoa huduma katika Halmashauri.
Viwango vya ada na ushuru vimeainishwa katika jedwari lenye sehemu A – I katika sheria ndogo hizi.
Adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo jera cha miezi sita itatolewa kwa mtu yeyote atakayevunja sheria ndogo hizi
Rasimu hii inawasilishwa katika kiakao hiki ili maoni yaweze kutolewa.

Naomba kuwasilisha.